# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 19 | Januari 8, 2022 NAKALA BILA MALIPO


# VITA BARIDI

**Vita vya maneno vya hivi majuzi kati ya Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja na Naibu Rais Rigathi Gachagua huenda vikawa ni mwanzo tu wa mzozo wa mamlaka unaotokota katika serikali ya Kenya Kwanza**



# The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore

## anywhere, anytime.

Follow the link to subscribe
> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play




Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111
Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

# Yaliyomo

**6 HALI TETE KENYA IKIFIKA MIAKA 60:** Huku IMF ikitabiri kuwa Afrika Mashariki itarekodi ukuaji wa haraka barani, Kenya bado inakumbwa na changamoto nyingi inapokaribia kuadhimisha miaka 60.

**9 SAKAJA HAFAI KUOGOPA:** Gavana wa Kaunti ya Nairobi amekosolewa vikali kwa kutoa maagizo ambayo hayakufurahisha eneo la Mlima Kenya, lakini, anafaa kukaa ngumu na kueleza wazi kuwa anawajibika kwa watu wa Nairobi pekee.

**11 KARATA KUBWA YA WAZIRI MKUU WA LIBYA:** Waziri Mkuu Ddeibah atarajia ushirikiano mwema na Amerika baada ya kumtoa mshukiwa wa mkasa wa bomu Lockerbie.



**13 BIBI AEGEMEA KULIA ZAIDI:** Kurejea kwa Netanyahu katika uongozi wa serikali yenye msimamo mkali zaidi katika historia kumezua tumbojoto katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na Mahakama ya Uhalifu ya Kimataifa mjini The Hague.

*- Zimetafsiriwa na Benson Matheka*

# Kampeni za mapema, maslahi ya kisiasa hazifai kutangulia utumishi kwa umma

Siasa zisizokoma zimekuwa kizingiti kikubwa kwa ufanisi wa kiuchumi wa Kenya. Kando na taharuki ya kisiasa - na wakati mwingine ghasia- zinazoshuhudiwa kabla, wakati na baada ya kila uchaguzi mkuu, ukweli ni kuwa nchi inatumbukizwa katika kampeni punde tu matokeo ya uchaguzi yanapotangazwa huathari vibaya ukuaji wa uchumi.

Mnamo 2002, Wakenya walitajwa kuwa watu wenye matumaini zaidi ulimwenguni baada ya serikali ya Muungano wa Rainbow Coalition iliyoongozwa na Rais Mwai Kibaki kuingia mamlakani.

Sifa nzuri ambazo nchi ilipata ulimwenguni, hata hivyo, ziliharibiwa rais alipozungukwa na watu walioweka mbele maslahi ya kibinafsi hatua ambayo ilisababisha ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa 2007.

Baada ya uchaguzi huo uliozua ubishi mnamo 2007, nchi ilikumbwa na msukosuko uliogawanya serikali ya muungano ya Bw Mwai Kibaki na kiongozi wa ODM Raila Odinga.

Mambo yaliimarika kiasi baada ya kuzinduliwa kwa Katiba ya 2010, ambayo iliunda Mahakama ya Upeo kama mpatanishi wa kutegemewa wa uhasama mkali unaofuatia kila uchaguzi. Mahakama hiyo ya upeo, hata hivyo, haikufaulu kukomesha ghasia za baada ya uchaguzi.

Baada ya uchaguzi wa urais wa 2017, kwa mfano, upinzani ulisusia uchaguzi wa marudio ulioagizwa na Mahakama ya Upeo na ukamtangaza kiongozi wake "rais wa watu", na kuzidisha msukosuko wa kisiasa ambao ulivuruga kwa kiwango kikubwa uchumi wa nchi.

Kinachosababisha mkasa huu wa kampeni zisizokoma ni ukweli kwamba maafisa wakuu wa serikali hutumia muda mwingi katika kampeni, wakigeuza umakinifu wa umma kutoka kwa ajenda ya maendeleo ya nchi.



Henry Munene

**Kinachosababisha mkasa huu wa kampeni zisizokoma ni ukweli kwamba maafisa wakuu wa serikali hutumia muda mwingi katika kampeni, wakigeuza umakinifu wa umma kutoka kwa ajenda ya maendeleo ya nchi.**

Hatari ya aina hii ni kubwa hata sasa, wakati ambapo tofauti na utaratibu wa majuzi wa kuajiri wataalamu kushikilia nyadhifa za mawaziri, wanasiasa wanatawala nyadhifa kuu serikalini, ambazo kwa kawaida watataka kuzitumia kujijenga ili kuingia katika nyadhifa za kuchaguliwa katika uchaguzi mkuu ujao.

Hivi ndivyo mambo yanavyoonekana kuwa katika serikali ya Kenya Kwanza, ambapo vigogo, kwa kujifanya wanaunganisha watu wao kuunga mkono serikali iliyo mamlakani, wanatumia muda mwingi kuweka mikakati ya kuingia katika ofisi kubwa na ushawishi mwingine wa mamlaka na kujifaidi wao binafsi.

Mfano mzuri ni malumbano kati ya washirika wa Naibu Rais Rigathi Gachagua na wa Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja. Kwa mtazamo rahisi tu, inaweza kuonekana kama ushindani wa kudhibiti masuala ya kibiashara ya jiji.

Hata hivyo, kama wachanganuzi wenye makini wanavyoeleza kwingine katika toleo hili, inazidi kubainika kuwa mzozo unaoonekana kuwa wa kikabila kati ya viongozi wa Mlima Kenya na Magharibi mwa Kenya ni dalili kuwa huenda kampeni za mapema za uchaguzi mkuu wa 2027 na urithi wa Ruto 2032 zimeanza.

Hatari iliyopo ni wazi kabisa. Kwa kumuonya Bw Sakaja kuachana na hatua ambazo ni juhudi za kupongezwa za kuondoa msongamano jijini, Bw Gachagua, anayeshikilia cheo cha pili kikubwa katika serikali ya Kenya Kwanza, anavuruga ajenda muhimu ya serikali, akitaka kuonekana kutetea maslahi ya watu wa eneo lilelo na watu wengi na hivyo lenye kura nyingi la Mlima Kenya kabla ya uchaguzi mkuu wa 2027.

Ukiruhusiwa kuendelea, mtindo huu una uwezo wa kupanda mbegu za chuki za kisiasa na kulemaza ajenda ya maendeleo ya Rais Ruto.

Ili kuepuka hali hii, Rais, ambaye amerudi kutoka kwa mkutano wa kikazi na maafisa wakuu wa serikali, lazima aweke nidhamu katika Baraza lake la Mawaziri.

Ni lazima awaeleze wazi kuwa utoaji wa huduma haufai kuvurugwa na maslahi ya kieneo na ya kibinafsi.

***hmunene@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Darubini ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Joe Ageyo** Mkurugenzi wa Uhariri
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Apu kuchunguzwa kwa shughuli haramu




# TikTok: Taiwan yahofia usalama

Mmiliki wa TikTok ambaye ni raia wa China Jumatatu alikana kuwa amefungua kampuni nchini Taiwan, baada ya idara za serikali katika kisiwa hicho kusema zimeanza kuchunguza mtandao huo kwa "kuendesha shughuli haramu."

Baraza la Kusimamia Masuala ya Bara (MAC), ambalo hubuni sera nchini humo, lilisema baraza la mawaziri liliagiza uchunguzi wa kuhusu changamoto za kiusalama zinazotokana na matumizi ya TikTok. Mkutano huo ulifanywa mapema mwezi huu.

Kesi hiyo pia iliwasilishwa kwa viongozi wa mashtaka kuchunguzwa, baada ya kampuni moja nchini humo kudaiwa kuendesha biashara Taiwan kwa niaba ya kampuni ya ByteDance, inayomiliki TikTok nchini China, ikasema MAC.

Majukwa ya intaneti na mitandao ya kijamii nchini China yamepigwa marufuku kufanya biashara Taiwan. Jumatatu, ByteDance ilisema haina shughuli zozote Taiwan. "Ripoti za majuzi zinazosema ByteDance imefungua tawi nchini Taiwan si za kweli," msemaji akaambia AFP. "Kampuni hiyo haijafungua biashara zozote halali nchini Taiwan."

TikTok inapatikana nchini Taiwan lakini si maarufu sana. Gazeti la 'Liberty Times' liliripoti Jumatatu kuwa kampuni inayochunguzwa ilianzishwa 2018 na ikabadilisha jina lake kuwa ByteDance Taiwan Ltd Co mnamo Novemba.

Taiwan imeonya kwa muda mrefu kuwa imeteseka kutokana na kampeni za kupotosha na shughuli za kijasusi zinazoendeshwa na China dhidi yake.

■ Ndiye mchezaji ghali wa majuzi zaidi

# Wasaudi wapigania jezi za Ronaldo

Saa chache tu baada ya Cristiano Ronaldo kutia saini mkataba wa miaka miwili na klabu ya Al Nassr nchini Saudi Arabia, umati wa watu ulielekea katika duka la kuuza mavazi ya kandanda jijini Riyadh na kununua jezi mpya za mwanasoka huyo.

Abdulmohsen al-Ayyban, 41, na mwanawe wa miaka tisa, Nayef, walikuwa miongoni mwa watu waliopiga foleni katika duka la klabu ya Al Nassr la kuuza mavazi ya michezo Jumamosi kununua jezi zenye jina la Ronaldo. "Tunashuhudia hali ya kihistoria," al-Ayyban akaambia AFP kuhusu mkataba huo ambao anaamini "utainu ligi ya kandanda Saudi Arabia".

Mnamo Ijumaa, Ronaldo alitia saini mkataba na klabu ya Al Nassr hadi Juni 2025 unaoaminika kuwa wa zaidi ya Sh26 bilioni. Nayef alionekana mchangamfu alipovaa jezi hiyo. "Nimekuwa nikitamani Al Nassr ipate mwanasoka bora duniani," akasema. "Nitahakikisha ninatazama mechi zake zote uwanjani."




Cristiano Ronaldo apozi na jezi ya klabu ya Al Nassr jijini Madrid Desemba 30, 2022 baada ya kutia saini mkataba.

Ronaldo, 37, anatarajiwa kujitokeza mbele ya mashabiki Alhamisi ijayo. Kwa Saudi Arabia, Ronaldo ndiye mchezji wa juzi zaidi kununuliwa kwa bei ghali ili kuongezea umaarufu wa nchi hiyo kimataifa.

Nyumbani, mkataba huo ulionekana kuongeza furaha iliyokuwepo baada ya timu ya kandanda ya falme hiyo kuishinda Argentina katika hatua za mwanzo za Mashindano ya Kombe la Dunia 2022, ushindi uliotajwa kuwa nadra katika historia ya mashindano hayo.

Watu walianza kufurika katika duka la Al Nassr baada ya ripoti kuhusu mkataba huo kufichuliwa na vyombo vya habari Ijumaa usiku - saa chache kabla ya tangazo rasmi.

Abdulqader, meneja wa duka hilo, alisema foleni zilitoka nje ya duka hilo na zimekuwa zikiongezeka tangu wakati huo.

Jezi hizo zilielekea kuisha na kulazimu wateja kupeleka zao wenyewe kuandikwa jina la mchezaji huyo – kazi ambayo itachukua hadi siku mbili.

■ Vikao vya kamati kuanza tena wiki hii

# Wabunge warudi baada ya likizo



Wabunge wanatarajiwa kuanza tena vikao vya kamati katika Bunge wiki hii baada ya kupumzika kwa zaidi ya mwezi mmoja kutokana na likizo ndefu ya Desemba.

Mabunge yote mawili - Bunge la Kitaifa na Seneti - yalienda likizo Desemba 2, 2022 na yatarudia vikao vya kawaida Februari 14, 2023.

Lakini mikutano ya kamati, ilisimamishwa Desemba 19, 2022 kwa Bunge la Kitaifa na Desemba 9 kwa Seneti, itaanza mwezi mmoja mapema.

Kamati hizo huwa nguzo muhimu katik utendakazi wa mabunge katika kutathmini utungaji sheria, kutathmini na kupitisha bajeti na matumizi.

■ Machifu pia watapewa silaha

# Polisi wa akiba kupiga vita ujambazi



Serikali wiki hii itaanza kurudisha polisi wa akiba (NPR) katika maeneo 14 yanayokumbwa na visa vya ujambazi walikoondolewa na serikali iliyopita.

Waziri wa Usalama wa Ndani Profesa Kithure Kindiki alitoa tangazo hilo wiki iliyopita baada ya watu wawili kuuawa na majambazi wenye silaha katika Kaunti Ndogo ya Marakwet Mashariki.

Waziri pia aliamuru polisi hao wapewe silaha mara moja ili kukabiliana na tatizo hilo huku serikali ikiendelea kuongeza idadi yao.

Kama sehemu ya mpango huo, machifu watapewa silaha na angalao polisi watano kuwasaidia kuimarisha usalama katika maeneo hayo.

*- Zimetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MIELEKA YA MAMLAKA

# VITA BARIDI VYA WAKUBWA

## Uhasama kati ya wanasiasa wa Magharibi na Mlima Kenya unaashiria vita vya ubabe

Na COLLINS OMULO

Vita vya maneno vinavyoendelea kati ya viongozi wa kisiasa kutoka maeneo ya Magharibi na Mlima Kenya vinaendelea kufichua ushindani wa ubabe wa kisiasa kati ya Naibu Rais

Rigathi Gachagua na Mkuu wa Mawaziri Musalia Mudavadi.

Matamshi ya hadharani yanaonyesha vita vikubwa baridi kati ya vigogo hao wawili wa maeneo, wote wakiwa na azima fiche ya kuongoza nchi hii miaka ijayo.

Kilichoanza kama Naibu Rais kumuonya Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja kuhusu mipango yake ya kuhamisha matatu kutoka katikati mwa jiji sasa kimegeuka kuwa vita chafu vya kisiasa kati ya viongozi wa maeneo hayo mawili.

Ushindani unaotokota wa kikabila na kujipiga kifua kisiasa ni vita vikali vya kuvutia umakini wa Rais Ruto vikilenga uchaguzi wa 2027. Mgogoro kati ya Naibu Rais na gavana ni zaidi ya udhibiti wa masuala ya jiji.

Gachagua ni wa pili kwa mamlaka na mrithi mtarajiwa katika utawala wa Ruto, huku kiongozi Amani National Congress (ANC) Musalia Mudavadi akitangaza wazi kuwa ameahirisha tu ndoto yake ya urais kwa sasa.

Mchanganuzi wa siasa Javas Bigambo anasema Gachagua anataka kujaza pengo la uongozi lililoachwa katika eneo la Mlima Kenya baada ya Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta kuacha siasa. Hii, anaeleza, ndiyo sababu Mbunge huyo wa zamani wa Mathira anataka kuonekana anatetea maslahi ya kiuchumi na kisiasa ya eneo hilo.


Kulingana na Bigambo, mzozo wa Gachagua na Sakaja ni sehemu ya mpango wa kuonyesha kuwA Naibu Rais anajali maslahi ya wafanyabiashara matajiri eneo hilo.

Huu, anaongeza mchanganuzi huyo, ni mkakati mwafaka wa kuvutia waliounga mkono muungano wa Kenyatta na Raila Odinga kuelekea uchaguzi wa Agosti 9.


"Shabaha ya Gachagua si Sakaja. Nia yake hasa ni kujijenga kisiasa na kufaidi kutokana na hatua hiyo," anasema Bw Bigambo.



Musalia Mudavadi



Johnson Sakaja



Rigathi Gachagua

Pili, mchanganuzi huyo anaeleza, Naibu Rais anataka kumuondolea shaka Rais Ruto kuwa ndiye anayefaa kutegemea katika kuungwa mkono na Wakikuyu.

Mnamo Oktoba mwaka jana, Rais Ruto alijitangaza mbabe wa kisiasa wa Mlima Kenya. "Nawakaribisha katika mlima, lakini hata wanapokuja, nataka wajue mlima ina wenyeji.

Walipokuwa kwingine, nilizuru eneo hilo mara kadhaa, tukajenga barabara na kuzindua miradi mingine ya maendeleo," akasema Ruto katika shule ya msingi ya Nyahururu DEB Kaunti ya Laikipia.

Gachagua sasa anajionyesha kuwa asiyeweza kushindwa kwa ushawashi katika eneo hilo.

"Gavana Sakaja ni kisingizio tu. Suala hapa ni kuwa Ruto aliienda eneo la Kati kabla ya kukutana na Gachagua. Je, 2027 atafanya alivyofanya kwa usaidizi mdogo wa Gachagua au atamchukulia kuwa mgombea mwenza asiyepingwa kwa sababu atakuwa amejijenga kuwa mbabe wa kisiasa wa eneo la Kati ya Kenya?" aanauliza Bigambo.

Kwa sababu ya cheo chake, Naibu Rais ndiye mwanasiasa mkuu kutoka eneo la Mlima Kenya na amekuwa akitembea kote eneo hilo akijaribu kuunganisha viongozi wote waliochaguliwa.

Amekuwa akiwarai viongozi wa muungano wa Azimio kutoka eneo hilo wajiunge na upande wake akiapa kuhakikisha hakutakuwa na migawanyiko ya kisiasa kati ya Mlima Kenya Mashariki na Magharibi. "Tutaunganisha eneo letu, Mlima Kenya, ili tuzungumze kwa sauti moja," alisema.

Gachagua pia amerai Wakfu wa Mount Kenya, kundi la mataji wa Mlima Kenya ambao inasemekana walifadhili kiongozi wa Azimio Raila Odinga kabla ya uchaguzi mkuu wa Agosti 9, ili waunge mkono serikali ya Kenya Kwanza.

Akihojiwa na NTV mnamo Septemba mwaka jana, Gachagua alisema: "Kwani msemaji ni nini? Ninachojua ni kuwa mimi ni Naibu Rais wa Jamhuri ya Kenya na mimi ndiye kiongozi mkuu zaidi kutoka eneo hilo. Kwa hivyo, jinsi watu wanavyonichukulia, ninawaachia waamue, lakini ninachojua ni kuwa ninazungumza na watu wa Mlima Kenya kwa lugha yao na wananisikiliza."

Amekuwa pia msitari wa mbele katika juhudi za kuleta muafaka wa kisiasa kati ya madiwani wa Meru na gavana wao wanayempiga vita, Kawira Mwangaza, katika kile kinachoonekana kuwa mkakati wa kukita mizizi katika sehemu hiyo ya nchi.

Kwa upande mwingine, Mudavadi amekuwa akijaribu kuunganisha ngome yake ya Magharibi nyuma yake. Kwa kufanya hivyo, makamu rais huyo wa zamani amefanya mikutano kadhaa na viongozi waliochaguliwa wa eneo hilo, ambayo imetafsiriwa kuwa sehemu ya kuunganisha eneo hilo nyuma yake kabla ya uchaguzi mkuu wa 2027.

Mbunge wa Sirisia John Waluke, wa chama cha Jubilee, ambaye pia ni mwenyekiti wa Kundi la Wabunge kutoka Magharibi mwa Kenya alisema kundi hilo linataka kurudisha umoja wa Waluhya, jamii ambayo imekuwa vigumu kuungana tangu uhuru.

Katibu Mkuu wa Muungano wa vyama vya wafanyakazi Francis Atwoli pia amekuwa akiunga wazo la viongozi kumuunga mkono Mudavadi, ambaye anachukuliwa kuwa kiongozi mkuu zaidi kutoka eneo la Magharibi na ambaye amehudumu kama makamu rais, ameshikilia nyadhifa tofauti za uwaziri, na pia aligombea urais mnamo 2013.

Mnamo 2017, Mudavadi alimuunga mkono Raila kugombea urais kwa tiketi ya uliokuwa muungano wa National Super Alliance (Nasa) ilhali 2022 aliacha azma yake ya urais na kumuunga mkono Ruto.

Sakaja aliunga mkono azma ya urais ya Mudavadi kuelekea uchaguzi mkuu wa Agosti 9, 2022, kabla ya ANC kuungana na UDA.

Hivi majuzi, Gachagua aliambia gavana huyo wa jiji kuwa ndiye (Gachagua) aliagiza watu wa jamii yake kumpigia (Sakaja) kura. Alimtaka Sakaja awe akishauriana naye kuhusu masuala yanayoweza kuathiri biashara katika jiji.

Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Mzozo unaotokota

Kutoka Uk 5

Mgawanyiko baridi kati ya Naibu Rais na Mkuu wa Mawaziri umevutia viongozi wa maeneo ya Mlima Kenya na Magharibi.

"Baada ya kupata vyeo vipya, Kwa sababu ya kuwa na afisi zao mpya, azma zao zimefufuka kwa sababu Rigathi anahisi hayuko mbali na kuwa rais, huku Mudavadi akiona nafasi ya kuwa rais pengine 2027 au 2032. Wanataka kutumia nyadhifa zao kujijenga upya," anasema Profesa Masibo Lumala wa Chuo Kikuu cha Moi.

Onyo la Naibu Rais kwa Sakaja limelaaniwa na viongozi wa eneo la Magharibi mwa Kenya.

Mbunge wa Bumula Jack Wamboka alitishia kuwasilisha mswada wa kumtimua Gachagua Wabunge wakirudia vikao Februari 13: "Nimekusanya sahihi za kutosha na punde tukirudia vikao mwezi ujao, nitatoa ilani ya mswada wa kumuondoa afisini. Hatuwezi kuwa na kiongozi anayesumbua Wakenya."

"Musalia amekuwa na tabia nzuri kuliko Naibu Rais," akasema Wamboka. "Kila mara Gachagua anapofungua mdomo wake, unashangaa iwapo ni Naibu Rais (wa Kenya) au ni Naibu Rais wa jamhuri ya Wakikuyu. Ameanza kuwa fedheha kubwa kwa nchi hii," akasema Mbunge huyo.

Gavana wa Kakamega Fernandes Barasa naye alisema: "Naibu Rais Gachagua anafaa kuheshimu Katiba. Gavana Sakaja anasimamia Kaunti ya Nairobi. Aache afanye kazi yake bila kuingiliwa."

Vitisho vya kumtimua Gachagua vilishutumiwa vikali eneo la Mlima Kenya.

"Kama hawawezi kuungana kupiga kura kama eneo, watawezaje kuungana kumuondoa Naibu Rais?" akashangaa Mbunge wa Mathira Eric Wamumbi.

"Ndiyo, Naibu Rais ni kiongozi wa kitaifa, lakini pia kuna mahali anakotoka. Kama Naibu Rais, ndiye kiongozi wa jamii ya Wakikuyu. Kwa hivyo, anapohisi watu wetu wanatishiwa, ni lazima azungumze jinsi tu Mudavadi anavyoweza kufanya kwa niaba ya watu wa Magharibi."

Gavana wa Nyeri Mutahi Kahiga alimwambia Bw Wamboka athubutu kuwasilisha mswada wa kumtimua Gachagua akisema "tuko tayari zaidi".

Kwa upande wake, Sakaja anasisitiza kuwa hatabadilisha ajenda yake ya maendeleo, akisema anaungwa mkono na Rais Ruto.

"...Nilisikia mtu akisema .... 'oooh Sakaja, hii Nairobi ilikuwa hivyo kabla hujazaliwa', lakini hiyo ndiyo sababu mimi ni Gavana ... siwezi kuacha iwe ilivyokuwa kabla sijazaliwa," akasema Bw Sakaja.

"Mabadiliko ni magumu lakini hayaepukiki ... ni lazima tubadilishe jiji letu ... ling'ae kama johari katika Bara la Afrika," akaongeza.

Vita baridi kati ya Naibu Rais Gachagua na Bw Mudavadi vilianza punde tu baada ya ANC kuungana na UDA na Ford Kenya kuunda muungano wa Kenya Kwanza.

"Ninavyojua mimi, Ruto ni mgombea urais, na mgombea mwenza atatoka Mlimani wakati wa kumteua ukifika. Wadhifa wa Bw Mudavadi unaendelea kujadiliwa. Hatakuwa mgombea urais na ninaweza kuthibitisha hilo," alisema Bw Gachagua mnamo Februari 2022.

"Walipojiunga nasi (ANC na Ford Kenya), tayari tulikuwa tumefanya majadiliano mengi, na tuliwaambia kwa sababu sisi ni watu waaminifu," akaongeza.

Ili kuepuka taharuki ya kisiasa, Rais Ruto aliunda afisi ya Mkuu wa Mawaziri, ingawa baadhi ya majukumu ya afisi hizo mbili yanafanana, huku wadadisi wa siasa wakisema ilikuwa hatua maksudi ya rais kuhakikisha wawili hao wana "shughuli nyingi".

Bw Mudavadi na Bw Gachagua wamekuwa wakiwakilisha Rais katika hafla tofauti.

Mbunge wa Kimilili Didmus Barasa alisema kuwa wanaosema Bw Mudavadi anamezea mate wadhifa wa Naibu Rais Gachagua 2027 "hawaelewi" uhusiano wa kisiasa kati ya wawili hao.

"Dhana ya kuwepo kwa vita baridi kati ya wawili hao inaendelezwa na mayatima wa Azimio wanaotaka kuendelea kusikika," akasema mbunge huyo.

***comulo@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

■ MIAKA 60 YA UHURU

## Suala kuu 2023 litakuwa uchumi

# HALI TETE KENYA IKIWA MIAKA 60




• Na KWENDO OPANGA

Kenya itakuwa na umri wa miaka 60 mwaka huu. Na ingawa itafikisha umri huo mwishoni mwa 2023, viongozi wake, hasa wnaotoa wito wa mabadiliko kila wakati wa uchaguzi, na wananchi kwa jumla, huenda watataka kukaribisha mwaka huu kuwa wa kutathmini hali ya nchi tangu rais wa kwanza, Jomo Kenyatta, alipotuongoza kupata uhuru.

Si jambo la kushangaza kwamba huenda suala la uchumi likatawala siasa 2023. Wiki iliyopita, IMF ilibadilisha utabiri wake wa Julai iliyopita, kwamba uchumi duniani ungekua kwa asilimia 2.9, badala yake ikisema utashuka hadi asilimia 2.7.

Mkurugenzi Mkuu Kristalina Georgieva alitoa tathmini ya kusikitisha kuhusu uchumi duniani, ambapo huenda Amerika, Umoja wa Ulaya (EU) na China zikavuta thuluthi moja ya dunia katika kushuka kwa uchumi.

Wadadisi wa uchumi wa Afrika, na wengine duniani, walifuata mazungumzo hayo kwa wasiwasi. Mnamo Novemba, Benki ya Maendeleo ya Afrika ilitabiri kuwa chumi za ukanda wa Afrika Mashariki zingeimarika janga la corona lilipokuwa likiendelea kupungua duniani, mataifa kufungua chumi zake, usambazaji wa bidhaa kurudi hali ya kawaida na utalii kuimarika.

Benki hiyo inasema katika kiwango cha asilimia 4.7, uchumi wa Afrika Mashariki

ndio utakaokua kwa haraka sana ukilinganiswa na maeneo mengine.


Kituo cha kutathmini hali ya uchumi cha Economic Intelligence Unit kiliripoti kuwa uchumi wa Kenya ndio utakuwa kwa kasi zaidi katika eneo hili, kwa kiwango cha asilimia tano. Hii ni

baada ya Kenya kuepuka hofu zilizohusishwa na Uchaguzi Mkuu wa Agosti mwaka uliopita.

Huku dunia ikiendelea kushuhudia kudidimia kwa uchumi, Kenya itakuwa ikifuatilia kwa makini mapigano yanayoendelea nchini Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya kenya



Rais William Ruto akutana na Mkurugenzi Mkuu wa IMF Managing Kristalina Georgieva kando ya Kongamano la COP27 jijini Sharma El-Sheikh, Misri, mnamo Novemba 2022. PICHA | PCS

Kuongezeka kwa mojawapo ya vita hivyo kutahatarisha matumaini ya eneo hili kufufua uchumi wake.

Kenya inaongoza juhudi za kurejesha amani nchini DRC katika viwango vya kidiplomasia na kijeshi. Vikosi vya kijeshi kutoka Kenya, Uganda na Sudan Kusini vimeingia DRC huku mazungumzo yakifanywa katika jiji kuu la Kenya, yakiongozwa na Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta. Alitekeleza jukumu kama hilo katika mzozo wa Ethiopia.

Kenya pia itakuwa ikifuatilia hali ya hewa kwa sababu kaunti 31 kati ya 47 zinakumbwa

na kiangazi na njaa, hali ambayo imeacha mamilioni ya raia bila chakula na maelfu ya mifugo kufa. Mvua imekosa kunyesha kwa misimu minne mfululizo na hali hiyo ikiendelea itaondoa matumaini ya uchumi kufufuka.

Rais William Ruto pia atazingatia kuwa Benki ya Dunia ilipunguza utabiri wa ukuaji wa uchumi wa Kenya kutoka asilimia 5.5 hadi asilimia tano, ikitaja ukosefu wa kujitosheleza kwa

chakula na mfumuko wa bei wa bidhaa kuwa sababu ya utathmini huo mpya. Benki hiyo ilibadilisha utabiri huo tena Desemba kuwa asilimia 5.2.

Tayari, Rais alikuwa ameambia Bunge lipunguze matumizi kusaidia serikali kutenga pesa na kugharamia utekelezaji wa ahadi zake za kampeni.

Kwa serikali iliyofanya kampeni na kuchaguliwa kwa ahadi ya kuinua kiuchumi na kisiasa raia maskini ambao sasa wanajulikana kama mahasla, hali mbaya ya kiuchumi itakuwa pigo kubwa kisiasa dhidi yake. Rais Ruto na washirika wake watakuwa wakifuatilia kwa makini mkondo ambao mfumuko wa bei utachukua, ikizingatiwa kuwa umefikia kiwango cha asilimia 9.5.

Serikali imejitahidi kumaliza hofu za msukosuko wa kisiasa baada ya uchaguzi. Hali hiyo imetokana na kupingwa kwa matokeo ya uchaguzi na uvumi kuwa Rais Ruto ni mwanasiasa

mwenye kisasi anayeweza kugeuka kuwa dikteta. Mgombeaji urais aliyeshindwa, Raila Odinga, amekuwa akichochea madai hayo huku akidokeza nia yake ya kuongoza maandamano dhidi ya serikali.

Wakati huo huo, Odinga ameeleza wazi kuwa anapanga anachotaja kuwa vikao vya mashauriano na Wakenya kote nchini kuhusu hali ya nchi kupata maoni yao kabla ya kutangaza hatua ambazo upinzani utachukua. Akihojiwa na 'Darubini ya Wiki', mkuu wa

mawasiliano wa Odinga, Dennis Onyango alisema kuna uwezekano maandamano

hayo yataanza baada ya vikao hivyo.

Wadadisi wengi walitarajia kwamba Odinga angejiuzulu baada ya kushindwa kwa

mara ya tano katika uchaguzi wa urais Agosti iliyopita. Hata hivyo, kujitokeza kwake kama mhusika mkuu badala ya aliyekuwa Makamu wa Rais Kalonzo Musyoka, aliyemuunga

mkono, kunaendelea kushangaza marafiki na maadui wake.

Inaonekana iwapo Bw Musyoka, ambaye hapendi kushiriki maandamano atajimudu kisiasa na kumlazimisha kustaafu au iwapo Odinga, inavyodhaniwa na wengi, anajiandaa kuwania urais kwa mara ya sita.

Hata hivyo, ni wazi kuwa upinzani dhidi ya serikali utaendeshwa katika maeneo mawili makuu; katika Bunge, kupitia Wachache, na barabarani, kupitia Odinga na washirika wake. Rais anajiamini bungeni kwa sababu ana Wabunge wengi, lakini anahofia maandamano yanaweza kumzuia kutimiza ajenda yake.

Maandamano, mfumuko wa bei, gharama kubwa ya maisha au ya bidhaa za msingi, na njaa katika zaidi ya kaunti 30 ni hali ambazo zinazoweza kuchochea janga katika nchi yoyote ile duniani, kwani zinaweza kukwamisha uchumi. Na hali hiyo itaathiri juhudi za Kenya Kenya kutafuta amani ya kikanda, ambayo inategemea hali ya uchumi.

Akihojiwa kwa mara ya kwanza akiwa Waziri wa Mashauri ya Kigeni na Masuala ya Ughaibuni, Dkt Alfred Mutua aliambia 'Darubini ya Wiki' kuwa diplomasia ya Kenya imekitwa katika imani kuwa amani nchini DRC italeta nafasi kubwa kwa ukuaji wa uchumi wa eneo hili na bara Afrika ikizingatiwa kuwa nchi hiyo ina utajiri mkubwa mali asili.

Si ajabu kuwa Ruto na Mutua walimalizia masuala ya kidiplomasia mwaka uliopita jijini

Washington, ambako Rais Joe Biden aliandaa Kongamano la Viongozi wa Amerika na Afrika na kuahidi kutoa Sh6.7 trilioni kwa miaka mitatu ijayo. Lakini Mutua alikanusha akihojiwa na 'Darubini ya Wiki' kuwa Kenya inabadilisha Sera ya Kuegemea Mataifa ya Mashariki iliyotumiwa na Rais Mwai Kibaki na mrithi wake, Uhuru. Alisema serikali inapeleka Kenya kwa dunia wala si Mashariki (soma China) au Magharibi. Huenda Amerika ndiyo inabadilisha mwelekeo wake. Tovuti ya Africanews.com ilimnukuu Florizelle Liser, Afisa Mkuu Mtendaji na Rais wa Baraza Kuhusu Masuala ya Afrika akisema:

"Nafikiri, kwa Amerika, hatuelekezi mashirika ya kibinafsi. Hutamuona Rais wa Amerika akipeleka mashirika ya kibinafsi popote duniani, ilhali kwa nchi zingine, wakienda, (Rais Emmanuel) Macron, akienda huandamana na makampuni ya Ufaransa ili kufungua milango kwa biashara zao. Nafikiri hapa Amerika tunachukua mkondo huo kwa sasa."

Huenda Macron hakuwa katika fikra za Biden alipokuwa akifufua kongamano hilo la enzi za Obama, kwani wageni wengi barani Afrika hawajawa wakitoka Ufaransa, bali China. Na viongozi wa Ulaya, akiwemo aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza David Cameron na Chansela wa Ujerumani Angela Merkel, waliongoza jumbe za wafanyabiashara nchini China.

Amerika imefuata mkondo huo kwani imekuwa ikijikokota nyuma ya China, ambayo imejikuza kama mshirika wa kimaendeleo wa Afrika – ingawa wanadiplomasia wa Amerika, hasa katika serikali ya Rais Donald Trump, walitaja mikopo yake kwa serikali za Afrika kuwa diplomasia hatari. Walisema lengo la China ni kuyatwika mzigo wa madeni mataifa hayo na baadaye kutwaa utajiri wake. Deni la Kenya, ulipaji wake na athari zake kwa uchumi zitajitokeza sana


katika siasa za Kenya 2023 na, huku China na Amerika zikiendelea kutoa mikopo, pia zitaangaziwa sana masuala ya kiuchumi na kisiasa nchini, eneo hili na Afrika kwa jumla.

***kwendo58@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni




■ Wabunge na madiwani wakome kutumia vibaya utaratibu wa kuondoa viongozi

# Kumtoa afisa lazima iwe hatua ya mwisho



KWENDO OPANGA

Vumbi bado halijatulia katika jaribio la Bunge la Kaunti ya Meru la kumuondoa Gavana Kawira Mwangaza. Ushindi wake wa Agosti dhidi ya mwanasiasa mkongwe Kiraitu Murungi ulitikisa Kenya nzima. Sasa inasemekana kuna mpango wa kumuondoa Naibu Rais Rigathi Gachagua. Kupanda kwake haraka katika siasa za kitaifa kumezua utata.

Mnamo 2014, miezi michache baada ya Uchaguzi Mkuu mwaka uliongulia, Madiwani wa Kaunti ya Makueni walimzuia Gavana Kivutha Kibwana kuongoza kisha wakamuondoa. Kibwana aliwagonganisha madiwani hao na wananchi. Alimuomba Rais Uhuru Kenyatta avunjilie mbali kaunti hiyo. Kwa kifupi, Makueni ilipoteza zaidi ya mwaka mmoja katika siasa zisizo na maana.

Na Wakenya watakumbuka kuwa mnamo 2014, Mithika Linturi, akiwa Mbunge wa Igembe Kusini, sasa Waziri wa Kilimo, aliwasilisha hoja bungeni akilenga kumuondoa Waziri wa Ugatuzi, sasa Gavana wa Kirinyaga, Anne Waiguru. Linturi alikosa kufika bungeni kimakusudi alipotarajiwa kutetea hoja yake katika kikao cha bunge.

Inasikitisha kuwa madiwani wa Meru hawakujiandaa vizuri. Kamati ya maseneta 11 iliyopewa wajibu wa kuchunguza makosa aliyodaiwa kufanfa Kawira ilibaini kuwa hakuna hata shtaka hata moja lililothibitishwa. Lakini mwenyekiti wa kamati hiyo Seneta Boni Khalwale, kabla ya uamuzi huo, alitoa tamko muhimu.

"Hawakuhitaji, lakini unawahitaji," Khalwale alimwambia Kawira baada ya kamati yake kukamilisha uchunguzi. "Sijui utafanya nini," akasema, lakini, akakamilisha, "lazima utafute namna ya kufanya kazi nao." Madiwani walishinda, ingawa walipoteza! Bado watawinda na kujaribu kumuondoa kiongozi aliyechaguliwa ili akubali matakwa yao.

Kibwana, aliyeonekana na wenzake kuwa aliyefaulu kama gavana, alimshauri Kawira afanye kazi na madiwani hao. Anajua anachozungumzia. Lakini lazima Kawira akatae kushurutishwa, na kupalilia uhusiano mzuri kikazi na madiwani hao. Anafaa pia kuongea na Waiguru, aliyejipata katika hali hiyo muhula wa kwanza.

Vipi kwa Wabunge na Gachagua? Wabunge wasitumie vibaya mamlaka ya kumuondoa afisa wa serikali walivyofanya Linturi na madiwani. Moi alikuwa Rais wa mwisho kuteua na kufuta kazi Makamu wa Rais nchini alivyotaka. Kulingana na katiba ya sasa, Naibu Rais amechaguliwa na anawakilisha nchi. Kabla ya kumkabili, wanaopanga njama hiyo lazima wajiandae vilivyo.

Mzozo kati ya Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja na Gachagua haufai kutumbukiza Nairobi, hata si Kenya, katika machafuko. Sakaja hajakosea kwa kuondoa matatu katikati mwa jiji.

Gachagua naye hajakosea kwa kusema alishawishi Wakikuyu wampigie kura Sakaja. Kila mmoja wao anataka kujengea ngome yake ya kisiasa.

Naibu Rais hakumtishia Sakaja kisiasa, alisema anataka kukutana naye. Lakini alionekana kumwamuru Gavana wa jiji kubwa zaidi Afrika Mashariki na kitovu cha biashara, kukoma kusumbua wafanyabiashara Wakikuyu. Hili halikubaliki. Wafanyabiashara hawataamua jinsi biashara inavyoendeshwa Nairobi.

Serikali ya Kaunti ndiyo itaamua jinsi biashara itaendeshwa jijini. Kukiwa na mzozo kati ya biashara na Sakaja na wenzake, kuna mashirika ya kibinafsi, wataalamu wenye ujuzi, wasimamizi wa zamani na wataalamu kukutana na viongozi wa Kaunti kusuluhisha mambo. Kumuondoa afisa kunafaa kuwa hatua ya mwisho. Tafadhali waambie hilo Madiwani na Wabunge.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

■ Nairobi si mkoa wa jamii ya Mlima Kenya bali ni sura ya Kenya

# Sakaja anafaa kupinga vikali vitisho vya kikabila



MACHARIA **GAITHO**

Zaidi ya kuwa jiji kuu, makao makuu ya serikali na kitovu cha uchumi cha Kenya, Nairobi pia ni sura ya nchi hii; inaleta pamoja jamii zote, watu wa rangi tofauti, utamaduni, imani tofauti za kidini na raia wa nchi na matabaka tofauti.

Ni kituo cha kikanda na bara cha kibiashara na mawasiliano, na pia kinachopendwa na makampuni ya kimataifa, mashirika ya kimataifa ya maendeleo na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayohudumu katika eneo pana la Afrika mashariki na Kati. Nairobi hasa ni jiji la kimataifa, na maendeleo yake lazima yaonyeshe ukweli huo.

Gavana Johnson Sakaja alichaguliwa kwa ahadi ya kubadilisha jiji kuu kuwa la kiwango cha kimataifa linavyopaswa kuwa. Hii inamaanisha kuwa kwanza ni kurekebisha mambo madogo kama ukusanyaji wa takataka na utupaji wake, maji safi ya mfereji katika kila nyumba, mifumo ya maji taka, usambaji wa kutegemewa wa stima, uondoaji wa maji ya mvua, ujenzi na udumishaji wa barabara, afya na elimu, bustani za umma na maeneo ya kubarizi na mfumo wa uchukuzi wa umma unaofanya kazi vyema.

Kwa kuzingatia historia ya Nairobi na jinsi imekuwa ikisimamiwa vibaya miaka iliyopita na viongozi fisadi na wasiojua chochote, mambo hayo yanaweza kusikika kama yasiyowezekana.

Lakini kwa kujitolea na bidii, yanaweza kutekelezwa. Hakuna gumu kati ya yaliyotajwa hapo juu.

Kama gavana huyo kijana anaweza kukumbuka mambo au anafahamu historia, atagundua kuwa hafai kuunda chochote kipya lakini kufufua kilichokuwepo zamani jiji lilipokuwa sawa. Mengi ya mambo hayo yako chini yake huku majukumu mengine yakihitaji kushirikisha taasisi za serikali ya kitaifa, serikali za nchi jirani na watoaji huduma wa kitaifa.

Sakaja anaweza kushauriana na watu wengi wanaokumbuka enzi ambazo wakazi walihakikishiwa kuwa saa za takataka kuokotwa, na hawakuhitajika kulipa mara mbili, serikali na wanakandarasi wa kibinafsi.

Tunakumbuka enzi ambazo mabasi ya abiria yalikuwa yakisafiri kote jijini kabla ya machafuko ya wahudumu wasiodhibitiwa kuanza. Tunakumbuka zama zile ambazo kukatwa kwa maji na stima zilikuwa habari kuu, kabla ya mifumo kufeli na kuwa jambo la kawaida. Na wakati ambao wakazi walihakikishiwa elimu na huduma bora za afya katika vituo vya umma kabla ya hali ya sasa ya ubaguzi wa kiuchumi kuanzisha mifumo tofauti ya watawala na watawaliwa.

Haya ndiyo mambo anayofaa kuzingatia Sakaja kila anapoamka, lakini hataweza kuyatekeleza iwapo atavurugwa na siasa duni za kikabila na vitisho. Ni lazima asimame kidete na kuwaambia wazi wanaomhujumu kuwa Nairobi sio sehemu ya eneobunge la Mathira au sehemu ya eneo la Kati mashambani.

Wabunge kutoka Nyeri, Kiambu, Nyandarua au kaunti nyingine ya Mlima Kenya wanaodai wanazungumza kwa niaba ya Naibu Rais Rigathi Gachagua ni lazima wakome na kuacha mashambulizi yasiyofaa na vitisho dhidi ya Gavana wa Nairobi na kuzingatia maendeleo katika maeneo yao.

Ni kweli, Gachagua ana kila haki kufanya kila awezalo kujaza pengo la uongozi katika eneo lenye watu wengu la Mlima Kenya na pia kujikita kama msaidizi na pengine mrithi wa Rais William Ruto, lakini kuchochea mashambulizi dhidi ya Sakaja na kuhujumu juhudi zake za kusafisha jiji kuu hakufai kamwe.

Uongo kuwa juhudi za Sakaja za kuleta utulivu na mpangilio katika sekta ya uchukuzi na biashara ya uchuuzi zinahujumu wafanyabiashara wa Mlima Kenya jijini ni lazima utajwe ulivyo: kwamba ni uchochezi hatari wa kikabila ambao unaweza kuhujumu ugatuzi na mpango wa maendeleo wa serikali ya Kenya Kwanza.



Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja.
PICHA I LUCY WANJIRU

Kama Naibu Rais anatishwa na jukumu la Mkuu wa Mawaziri Musalia Mudavadi katika serikali ya Ruto, na vitisho anavyofikiria kuhusu ushawishi wake na mipango ya urithi wa urais, hafai kuelekeza mambo hayo kwa Gavana Sakaja lakini moja kwa moja kwa mtu anayelenga.

Pia, anaweza, kama ana ujasiri, kumkabili Rais Ruto na kumtaka afafanue kazi na majukumu yake na yale ya Mudavadi, badala ya kuchochea vita kwa mbali, hatua inayoonyesha jinsi serikali imegawanyika.

Sakaja alitia bidii kuwa gavana. Alihimili maswali makali kuhusu uadilifu na uaminifu wake katika kashfa kuhusu masomo yake kuhusu digrii yake kutoka Uganda.

Alilazimika kuunda muungano mpana ambao haukujua siasa duni za kikabila, kwa hivyo hakufaulu kwa sababu ya kuungwa mkono na Gachagua au mwanasiasa yeyote wa kijijini kutoka kaunti ya mbali mashambani.

Ni lazima gavana akae ngumu na kutangaza wazi kwamba anawajibika kwa watu wa Nairobi na sio kwa mtu mwingine. Haripoti kwa Gachagua, Mudavadi au hata Ruto.

Ni lazima pia adhihirishe kwamba ni "raia" na viongozi wa Nairobi watakaomuunga mkono dhidi ya mashambulizi yasiyo na msingi, na sio mbwa wanaobweka kutoka Vihiga au mahali pengine wanaodai kuongea kwa niaba ya Mudavadi au jamii yake ya Luhya.

Pia, itasaidia sana kama atapata kuungwa mkono hadharani na Rais Ruto. Kwa wakati huu, serikali ya Kenya Kwanza haifai kuonyesha migawanyiko ya viongozi wake.

Hakuna kitu ambacho Sakaja anafanya ambacho hakutaja katika ahadi zake za kampeni na pia katika manifesto ya Kenya Kwanza.

Kwa vyovyote vile, Nairobi sio mkoa wa jamii ya Mlima Kenya, lakini ni sura ya Kenya. Kwa hivyo, hakuna mpango wa maendeleo ambao utaathiri kabila moja na kuacha mengine. Uongo huu wa kusikitisha unafaa kuzimwa kabisa.

*gaithomail@gmail.com*


*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media


# habari kwa picha



Mwakilishi Alexandria Ocasio-Cortez akicheka ndani ya Ukumbi wa Bunge baada ya Bunge jipya kushindwa kuchagua Spika mpya katika Jengo la Bunge la Amerika la Capitol jijini Washington mnamo Januari 3, 2023 Washington. PICHA I AFP



Mwenyekiti wa Bodi ya BMW Oliver Zipse akielezea dhana ya gari jipya aina ya BMW i Vision Digital Emotional Experience EV jijini Las Vegas mnamo Januari 4, 2023. PICHA I AFP




LeBron James wa Los Angeles Lakers akicheza wakati wa mechi dhidi ya Charlotte Hornets katika ukumbi wa Spectrum Center mnamo Januari 2, 2023. PICHA I AFP




Mashabiki wa aliyekuwa nyota wa kandanda wa Brazil Pele wakusanyika nje ya uwanja wa Urbano Caldeira huku gari la zimamoto likisafirisha jeneza lake kwa Makaburi ya Kumbukumbu ya Santos jijini Santos, jimbo la Sao Paulo, Brazil, mnamo Januari 3, 2023, kabla ya kuzikwa katika kaburi maalumu. PICHA I AFP



Wagonjwa wa Covid-19 wapumzika kwenye vitanda katika Fengyang People's Hospital, Kaunti ya Fengyang, Mkoa wa Anhui mashariki mwa China mnamo Januari 5, 2023. PICHA I AFP



Msherehekeaji akishiriki gwaride wakati wa hafla ya "Weusi na Wazungu" jijini Pasto, Colombia, Januari 4, 2023, kusherehekea makabila tofauti katika eneo hilo. PICHA I AFP



Mwanamume akitoka kwenye kidimbwi cha Mto Songhua uliogandishwa na baridi eneo la Harbin Mkoa wa Heilongjiang, China, mnamo Januari 5, 2023. PICHA I AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"

# kurunzi ya afrika

■ MKASA WA NDEGE WA PAN AM

# LIBYA YAKABIDHI AMERIKA MSHUKIWA WA LOCKERBIE IKITARAJIA UPENDELEO



Kaimu Waziri Mkuu wa Libya Abdelhamid Dbeibah. PICHA I AFP

## Ddeibah anakabiliwa na shutuma kali kwa kupatia Amerika mshukiwa wa mkasa wa bomu katika kinachoonekana kuwa hatua ya kujipendekeza

• Tripoli, AFP

Serikali ya Libya jijini Tripoli inalaumiwa na umma kwa kukabidhi Amerika mshukiwa wa shambulizi baya la ulipuaji wa ndege mjini Lockerbie mnamo 1988, lakini inaamini uhusiano mwema na Amerika utaipatia nguvu dhidi ya maadui wake.

Shambulizi katika ndege ya Pan Am katika anga ya Scotland liliua watu 270, na kuwa baya zaidi la kigaidi kutokea Uingereza wakati amabo Libya ilikuwa chini ya utawala wa dikteta Moamer Kadhafi.

Mapema mwezi huu, anayedaiwa kuwa ajenti wa ujasusi Abu Agila Mohammad Masud Kheir al-Marimi alifikishwa katika mahakama ya Amerika akikabiliwa na mashtaka ya kutengeneza bomu lililotumika katika shambulizi hilo.

Anaweza kufungwa jela maisha akipatikana na hatia ya "kuharibu ndege na kusababisha kifo" na mashtaka mengine mawili yanayohusiana na hayo.

Hatua ya Libya kukabidhi Amerika Masud imesababisha lawama kwa serikali ya Abdulhamid Dbeibah, inayodhibiti Magharibi ya nchi ambayo inazongwa na mizozo na inapingwa na vikosi vya mbabe wa kijeshi Khalifa Haftar upande wa Mashariki.

Dbeibah amekosolewa vikali na wapinzani wa kisiasa, makundi ya kutetea haki na jamaa wa wafungwa wa Libya wanaohofia kukabidhiwa Amerika.

Khaled al-Montasser, Profesa wa uhusiano wa kimataifa katika Chuo Kikuu cha Tripoli alisema Dbeibah "pengine hatatoa mshukiwa mmoja tu – lazima wengine watafuata".

Baada ya kukiri kuwa mshukiwa huyo alikabidhiwa Amerika, Dbeibah alisema alifanya hivyo "kwa kuheshimu kikamilifu utukufu wa Libya".

Alikanusha uvumi kuwa anapanga kumkabidhi Abdallah Senoussi, ambaye alikuwa mkuu wa ujasusi wa Kadhafi wakati wa shambulizi hilo. "Senoussi hatakabidhiwa Amerika, yuko katika gereza lake Tripoli," Dbeibah

Endelea Uk 12

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Tripoli yakabidhi US mshukiwa ili kuungwa mkono

Kutoka uk 11

akaambia shirika la habari la Saudi Arabia, Al-Arabiya.

Mtu mmoja amehukumiwa kwa kulipua bomu ambalo liliua watu wote 259 waliokuwa katika ndege hiyo, wakiwemo raia 190 wa Amerika na watu wengine 11 ilipoanguka ardhini.

Serikali ya Libya ilifikiri kesi hiyo ilikuwa imefungwa tangu 2003 baada ya utawala wa Kadhafi kukiri rasmi kuhusika na shambulizi hilo, na kulipa dola $2.7 bilioni kama fidia na kukabidhi washukiwa wawili wa Libya.

Abdelbaset Ali Mohmet al-Megrahi na Al Amin Khalifa Fhimah walishtakiwa kwa ulipuaji huo wa bomu na kuhukumiwa na mahakama ya Scotland nchini Uholanzi. Megrahi alifungwa jela Scotland kwa miaka saba huku Fhimah akiachiliwa huru. Megrahi alifariki akiwa Libya mnamo 2012, na kila wakati alisisitiza hakuwa na hatia.

Lakini ingawa makubaliano ya 2008 yalikomesha suala la malalamishi ya kifedha ya fidia, "Amerika huwa haifungi kesi za uhalifu' zinazohusu raia wake, akasema Montasser.

Alisema serikali ya Biden inafufua suala la Lockerbie "ili kuwekea presha viongozi wa kisiasa wa Libya". "Hakuna afisa wa Libya angekataa" kumkabidhi Masud, akasema.

Mchanganuzi wa Libya Abdallah al-Rayes anashuku Dbeibah ana "mkataba wa kisiasa" na Amerika akilenga kupata usaidizi wake kukabiliana na maadui walio mashariki mwa Libya. "Viongozi wa Libya wanatarajia kurekebisha sifa zao" kwa Amerika na kutia nguvu nafasi yao huku kukiwa na uwezekano wa uchaguzi kufanywa 2023, akasema.

Aliongeza kuwa Dbeibah kuhalalisha hadharani kumtoa mshukiwa huyo "hakuridhishi kamwe," na kumeweka serikali yake katika hali mbaya. "Inaonekana kama iliyosaidia nchi ya kigeni," akasema.

Hata hivyo, Libya inahitaji uhusiano mwema na nchi zingine ulimwenguni ili iweze kuungwa mkono, kulingana na mchanganuzi Jalel Harchaoui. "Hizi sio shughuli za wazi na thabiti, lakini kampeni ya kubembeleza iliyoongozwa na familia ya Dbeibah hakika ni ya kweli," akasema Harchaoui.

"Dbeibah, ambaye umaarufu wake katika Libya umekuwa ukishuka jinsi muda unavyosonga, amegundua kuwa baadhi ya nchi za kigeni zinakubali kuendelea kwake kutawala kutoka mwezi hadi mwezi."


Ubalozi wa Amerika jijini Tripoli uliandika kwenye Twitter wiki jana kwamba "kuhamishwa kwa Masud hadi Amerika kwa kesi ya mashtaka yanayohusiana na kulipuliwa kwa bomu kwa ndege ya Pan Am 103 kulikuwa kwa kisheria na kulifanywa kwa ushirikiano na serikali ya Libya". Ulisisitiza kuwa haufungui upya makubaliano ya 2008 ambayo yalimaliza ufuatiliaji wa kisheria wa fidia ya kifedha katika mahakama za Amerika.

Hata hivyo, makubaliano hayo "hayazuii kwa njia yoyote ushirikiano wetu wa utekelezaji wa sheria au hauna uhusiano na mashtaka ya uhalifu dhidi ya waliohusika na shambulizi hilo," ukasema ubalozi huo.


*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*



**Raia wa Libya wakusanyika katika bustani ya Martyrs' Square katika mji mkuu wa Libya, Tripoli, mnamo Februari 18, 2022, kuadhimisha miaka 11 ya mapinduzi yaliyomtoa mamlakani kiongozi wa miaka mingi Muammar Gaddaffi.** PICHA I AFP



**Aliyekuwa kiongozi wa Libya Muammar Gadaffi** PICHA I GEOFFREY SSERUYANGE



**Abdelbaset Ali Mohmet al-Megrahi akiwa mjini Tripoli, mtu pekee aliyepatiakana na hatia ya kulipua ndege katika anga ya mji wa Lockerbie, Scottland, 1988.** PICHAI AFP

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya dunia

■ BENJAMIN NETANYAHU ARUDI MAMLAKANI

# BIBI AEGEMEA KULIA ZAIDI



Waziri Mkuu wa Israel na Kiongozi wa chama cha Likud, Benjamin Netanyahu, akihutubia wafuasi wake katika makao makuu ya kampeni jijini Jerusalem mapema Novemba 2, 2022, baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa kitaifa. PICHA I AFP

## Wasiwasi umezuka kote duniani kuhusu kile wachanganuzi wanataja kuwa serikali ya mrengo wa kulia zaidi katika historia ya Israel

● Jerusalem

Baada ya kipindi kifupi katika upinzani, Benjamin Netanyahu amerudi mamlakani nchini Israel, akiongoza kile wachanganuzi wanaelezea kuwa serikali ya mrengo wa kulia zaidi katika historia ya nchi hiyo.

Maafisa wakuu wa usalama tayari wameelezea hofu kuhusu hali hiyo, na pia Wapalestina. "Ni serikali waliyotaka washirika wa Natenyahu," Yohanan Plesner, rais wa wa Taasisi ya Demokrasia Israel akaambia AFP.

"Ni nzuri kwa upande mmoja na mbaya kwa upande mwingine," akasema, akiongeza: "Serikali hii inatarajiwa kupeleka nchi katika mkondo mpya kabisa."

Na siku moja tu baada ya utawala wa Bibi (anavyoitwa Netanyahu) kuchukua usukani, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) liliomba Mahakama ya Kimataifa Kuhusu Haki (ICJ) kuratibu adhabu kwa Israeli kwa kukalia maeneo ya Wapalestina.

Baraza hilo lilipiga kura 87 dhidi ya 26 kuunga mkono uamuzi huo huku mataifa 53 yakikosa kupiga kura. Ingawa mataifa ya Magharibi yaligawanyika kuhusu suala hilo, yaliunga mkono msimamo wa mataifa ya Kislamu - yakiwemo ya Kiarabu - ambayo yamerudisha uhusiano na Israel. Uamuzi huo pia uliungwa mkono na Urusi na China.

Uamuzi huo unaitaka mahakama hiyo ya The Hague ikadirie "matokeo ya kisheria kutokana na Israeli kuhujumu haki ya Wapalestina kujitawala". ICJ pia inatakiwa kukadiria mikakati iliyowekwa na Israel inayolenga kubadili idadi, hali na hadhi ya wakazi wa mji mtakatifu wa Jerusalem.

Balozi wa Palestina katika Umoja wa Mataifa Riyad Mansour alisema matokeo ya kura hiyo ni ishara kwa serikali mpya ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu kuhusu juhudi zake za "kuendeleza sera za kikoloni na kibaguzi". Aidha alipongeza mataifa yaliyokataa "vitisho na presha". "Tunaamini hata bila kura yake leo, ikiwa anaheshimu

Endelea Uk 14

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

# Hofu ya mwelekeo mpya wa Israel

Kutoka Uk 13

sheria ya kimataifa na amani, atakubali uamuzi wa Mahakama ya Kimataifa Kuhusu Haki utakapotolewa," akasema Mansour.


Akiongea kabla ya kura, Balozi wa Israel, Gilan Erdan, alitaja uamuzi huo kuwa "doa la kimaadili katika UN." "Hakuna shirika la kimataifa linaweza kuamua kuwa Wayahudi wanakalia kimabavu ardhi yao," Erdan akasema. "Uamuzi wowote kutoka kwa mahakama inayopata mamlaka yake kutoka kwa UN, isiyo na maadili na ambayo imeingizwa siasa, hautachukuliwa kuwa halali," akasema.

Uamuzi huo pia unaitaka Israeli kukomesha ujenzi wa makao. Lakini kura za Baraza Kuu hazina uzito kisheria - tofauti na zinazopigwa katika Baraza la Usalama, ambako mshirika wa Israel, Amerika, ana kura ya turufu.

Amerika, Uingereza na Ujerumani zilipinga uamuzi huo, ilhali Ufaransa haikupiga kura. "Hatuamini kuwa kuwasilisha suala hilo kwa Mahakama ya Kimataifa Kuhusu Haki kutasaidia kuwezesha pande husika kurudia mazungumzo," akasema Mwanadiplomasia wa Uingereza Thomas Phipps. "Pia ni msimamo wa Uingereza kuwa si sawa kuitaka mahakama kutoa ushauri kuhusu kile mzozo kati ya mataifa mawili bila idhini kutoka kwa pande husika," akaongeza.

Miongoni mwa nchi za Magharibi zilizounga mkono uamuzi huo ni Ureno, ambayo mwakilishi wake alitambua hatari ya "kutegemea sana mahakama katika mahusiano ya kimataifa" lakini akasema mahakama hiyo inaendeleza sheria ya kimataifa "ambayo tunalenga kulinda."

Netanyahu, 73, anayejitetea mahakamani kuhusu tuhuma za ufisadi, alikuwa waziri mkuu kwa muda mrefu kuliko mtu yeyote katika historia ya Israeli. Alihudumu kwa miaka 12 mfululizo, kutoka 2009 hadi 2021 na



Waziri wa Mashauri ya Kigeni wa Amerika Antony Blinken. PICHA | AFP

miaka mitatu mwishoni mwa miaka ya 1990.

Aling'olewa mamlakani 2021 na muungano wa vyama vyenye itikadi mbalimbali ulioongozwa na Naftali Bennett na aliyekuwa mtangazaji wa runinga Yair Lapid. Haikumchukua muda mrefu kabla ya kurudi.

Netanyahu aliwasilisha serikali yake mpya kwa bunge la Israeli kuidhinishwa baada ya uchaguzi wa Novemba 1. Alibuni ushirikiano na vyama vya kiothodoksi na vya mirengo ya kulia vikiwemo Religious Zionism cha Bezalel Smotrich na Jewish Power Party kinachoongozwa na Ben Gvir. Vyama hivyo viwili vina historia ya kutoa kauli kali kuhusu Wapalestina na sasa vitasimamia sera ya Israeli ya ujenzi wa makao eneo la West Bank na polisi wa Israeli, wanaohudumu eneo hilo ambalo limekaliwa na Israeli tangu 1967.

Hata kabla ya serikali hiyo kuapishwa, vyama vingi vilipitisha sheria zitakazoruhusu Aryeh Deri kutoka chama cha Shas Party kuhudumu kama waziri licha ya kuwa awali alipatikana na hatia kuhusu kosa la ushuru.

Vyama hivyo pia vilipiga kura kupanua mamlaka ya Waziri wa Usalama wa Kitaifa, wadhifa unaotarajiwa kupewa Ben Gvir atakayesimamia polisi. Hatua hiyo inachukuliwa licha ya Mwanasheria Mkuu Gali Baharav-Miara kuonya dhidi ya kuingiza siasa katika asasi za kisheria.

Katika simu aliyompigia Netanyahu Jumatatu, mkuu wa majeshi Aviv Kochavi alielezea hofu kuhusu kubuniwa kwa wadhifa mwingine wa uwaziri katika Wizara ya Ulinzi kutunikiwa Smotrich atakayesimamia masuala ya raia katika West Bank.

Waziri wa Mashauri ya Kigeni wa Amerika pia ameonya kuwa nchi yake itapinga kupanuliwa kwa eneo la makao na juhudi zozote za kutwaa West Bank. Lakini kwenye taarifa kuhusu sera zitakazopewa kipaumbele, iliyotolewa Jumatano, chama cha Netanyahu cha Likud Party kilisema serikali itaendelea na mpango wa upanuzi wa makao.

Walowezi 475,000 wa Kiyahudi wanaishi katika makao hayo yanayochukuliwa kuwa haramu kwa mujibu wa sheria ya kimataifa.

Wachanganuzi wanasema Netanyahu alitoa manufaa mengi kwa wanasiasa wa mrengo wa kulia kwa matarajio ya kupata kinga dhidi ya mashtaka au kuondolewa kwa keshi ya ufisadi inayomkabili. Ameshtakiwa kwa kutoa hongo, ulaghai na kukiuka uaminifu, madai ambayo amekana.

Denis Charbit, profesa wa sayansi ya siasa katika Chuo Kikuu cha Open University, aliambia AFP kuwa serikali "inazidisha udhaifu wa kisiasa wa Netanyahu, unaohusishwa na umri wake na mashtaka yanayomkabili, na hali kwamba una familia mpya ya wanasiasa wanamageuzi wa mrengo wa kulia yenye nguvu ambayo haijawahi kuonekana nchini Israel."

– AFP

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

# Wenye nguvu katika serikali ya Netanyahu

• Jerusalem

Ikiongozwa na Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu, anayerudi mamlakani baada ya kuwa nje kwa chini ya miaka miwili, serikali ya Israel inajumuisha mwanasiasa ambaye mwishoni mwa mwaka jana alikiri kosa la kukwepa ushuru. Inajumuisha pia mtu aliyeweka picha nyumbani kwake ya mwanamume aliyeua waumini kadhaa Wapalestina.

Hii ni orodha ya watu wanaoshikilia afisi kuu katika serikali ya 37 ya Israel.

Eli Cohen in baba ya watoto wanne na aliingia katika siasa 2015 kupitia chama kilichosambaratika cha Kulanu, kilichoegemea siasa za mrengo wa katikulia. Alijiunga na chama cha Likud miaka minne iliyofuata na Netanyahu akamteua waziri wa ujasusi 2020.

Cohen aliongoza mpango wa Israel ya kurudisha uhusiano mwema na Muungano wa Milki za Kiarabu (UEA), Bahrain na Morocco mwaka huo.

Waziri mpya wa Ulinzi, Yoav Galant, ni jenerali wa zamani wa jeshi, mshirika wa karibu wa Netanyahu na mtetezi sugu wa mpango wa ujenzi wa makao eneo la West Bank linalokaliwa na Israel.

Wakati mrefu aliokuwa katika jeshi, Galant, 64, aliongoza mpango wa Israel kuondoka katika Ukanda wa Gaza 2005 na baadaye akaongoza vita dhidi ya kundi la Hamas 2008 hadi 2009.

Mnamo 2015, Galant alikuwa waziri wa nyumba kupitia chama cha Kulanu, ingawa baadaye 2019 alijiunga na Likud cha Netanyahu. Alikuwa waziri wa uhamiaji na elimu kati ya 2019 na 2021.

Mzaliwa wa Morocco, Aryeh Deri ni mwanasiasa mkongwe aliyeshiriki kubuniwa kwa chama cha Shas na ameshikilia kiti cha bunge la Knesset kwa miaka 30 na pia nyadhifa kadhaa za uwaziri.

Mwishoni mwa mwaka jana, Deri alikiri kosa la kukwepa ushuru na baadaye akaahidi kulipa faini ya dola 50,000 (Sh6,000,000) kisha akajiuzulu. Awali, alifungwa jela kwa kosa la ulaghai. Lakini alishinda kiti katika uchaguzi wa ubunge wa Novemba na Jumanne bunge likapitisha sheria inayoruhusu mtu yeyote aliyepatikana na hatia lakini hajahukumiwa kifungwa jela kuhudumu kama waziri.

– AFP

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# Huawei yarudia shughuli zake licha ya vikwazo




• Beijing

Kampuni kubwa ya kiteknolojia nchini China, Huawei, Ijumaa ilisema imeanza tena "shughuli zake za kawaida" licha ya vikwazo ilivyowekewa na Amerika, huku ikikadiria kuwa mapato yake ya 2022 hayatabadilika.

Kampuni hiyo iliwekewa vikwazo wakati wa utawala wa aliyekuwa rais wa Amerika, Donald Trump, kuhusu usalama mtandaoni na hofu kuhusu ujasusi. Huawei inaongoza kwa utengenezaji wa vifaa vya mawasiliano, simu za rununu na mitambo mingine.

Mrithi wa Trump, Joe Biden, aliongeza vikwazo kwa kuweka masharti yanayotishia kampuni hiyo kupata nyaya maalumu za kutengenezea bidhaa zake.

Lakini mwenyekiti wa Huawei, Eric Xu, alitoa ujumbe wa kutia moyo katika hotuba yake ya Mwaka Mpya. "Mnamo 2022, tulifanikiwa kujitoa kwa mzozo uliotukumba. Kwa sasa, tumezoea vikwazo vya Amerika," akasema katika barua hiyo. "Tumerudi kwa shughuli zetu kama kawaida."


Kampuni hiyo ilitangaza mapato ya Sh11.1 trilioni mnamo 2022, kutoka Sh11.0 trilioni mnamo 2021. Huawei imechukua hatua kadhaa kupanua vyanzo vyake vya mapato baada ya vikwazo vya Amerika kuathiri pakubwa mapato yake ya uuzaji wa vifaa vya mawasiliano na simu.

Mitambo yake ya 5G imepigwa marufuku katika masoko makuu duniani, kama vile Amerika, Uingereza na Japan kuhusiana na hofu za kiusalama. Huawei hata hivyo imekana kuwa mitambo yake inakusanya maelezo ya kijasusi katika nchi zinazohusika.

*— AFP*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# TAIWAN KUUNDA KWA WINGI CHIPU ZA KISASA



• Tainan

Kampuni kubwa ya teknolojia ya Taiwan, TSMC, ilisema Alhamisi kuwa imeanza kuunda kwa wingi chipu za kisasa zaidi za urefu wa namometa 3 (3nm).

Taiwan Semiconductor Manufacturing Company hutengeneza chipu za utendaji wa juu zinazotumiwa katika simu za rununu, magari na makombora. Ndiyo pia inauzia chipu kampuni ya Apple.

Chipu zake za kisasa za 3-nm zinatarajiwa kuwa na nguvu huku zikitumia kiasi kidogo cha umeme na kuimarisha utendakazi wa betri.

"Teknolojia yetu ya 3nm itatumika sana katika vifaa ya kisasa vya kiteknolojia, kama vile kompyuta za kisasa, intaneti ya kasi ya juu na vifaa vingi aina ya simu za rununu," akasema mwenyekiti Mark Liu mjini Tainan akitangaza hatua ya kuanza kutengeneza chipu hizo kwa wingi.

Aliongeza kuwa kampuni hiyo inapanga kujenga vituo vya kutengeneza chipu ndogo hata zaidi za 2nm katika miji ya Hsinchu na Taichung. Kampuni ya Samsung kutoka Korea Kusini ilianza kutengeneza chipu aina ya 3nm mnamo Juni. Taiwan ina jukumu muhimu katika utengenezaji wa chipu duniani. TSMC pekee hutengeneza karibu asilimia 50 ya chipu za chini ya nanometa 10.

Kuwepo kwa viwanda hivyo katika eneo moja kumezua hofu ya kisiasa, hasa China inapoendelea kutishia Taiwan, taifa huru ambalo Chama cha Kikomunisti cha China kimeapa kulitwaa siku moja.

Uhaba wa chipu duniani wakati wa janga la virusi vya corona ulizidisha hofu hiyo. TSMC imekuwa ikishinikizwa na mataifa ya magharibi kujenga viwanda vingi duniani, wito ambao imekubali.

Kampuni hiyo inajenga kiwanda kikubwa cha Sh4.9 trilioni katika jimbo la Arizona, ambacho hatimaye kitatengeneza chipu za urefu wa 4nm na 3nm, ambao ni mpango wa Amerika wa kuhakikisha kuna chipu za kutosha katika himaya yake.

Rais Joe Biden alihudhuria hafla mapema mwaka huu kutangaza upanuzi wa kiwanda cha Arizona, ambacho ni miongoni mwa vikubwa vya kigeni nchini humo.

TSMC pia imekubali kujenga viwanda nchini Japan huku ikifikiria pia kufungua kingine nchini Ujerumani. Wakati huo huo, kampuni za kiteknolojia nchini Taiwan na serikali yake zinalenga kuhakikisha utengenezaji wa chipu za kisasa zaidi umebakia nchini humo, mojawapo ya sababu ikiwa kwamba biashara hupatia kisiwa hicho kinga fulani.

Hatua yoyote ya China kuivamia Taiwan itazua athari kubwa kwa uchumi duniani kwani chipu muhimu hutengenezewa humo – hali inayowafanya wachanganuzi kuitaja Taiwan kuwa "Ngao ya Silicon."


Rais Tsai Ing-wen amepuuzilia mbali hofu kuwa huenda Taiwan ikapoteza kinga hiyo - na ajira - kwa kujenga viwanda ugenini, akisema badala yake, hilo limeonyesha ushupavu wa kisiwa hicho katika masuala ya teknolojia.

"Mwanzilishi wa TSMC Morris Chang amesema mara kadhaa kuwa Taiwan ndiyo nchi bora kwa TSMC kuwekeza kwani ina mazingira mazuri na kiwango cha juu cha nguvu kazi," akasema Tsai mapema wiki hii. "Alimaanisha kuwa hatupaswi kuwa na wasiwasi kuhusu sekta ya chipu nchini Taiwan."

*— AFP*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media


SPORT ON!
JAMES WOKABI
BERNARD NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM